# TAARIFA YA MIKUTANO YA KANDA YA WADAU WA KAHAWA

**na**

**Kamati za Kanda**

# Utangulizi

- Mikutano ya Kanda ya wadau wa kahawa imefanyika katika Kanda zote za uzalishaji wa kahawa kabla ya kufanyika kwa mkutano huu Mkuu
- Mikutano hii inafanyika ili kutoa fursa kwa wadau wa kila eneo la uzalishaji kujadiliana changamoto zinazokabili sekta ya kahawa na fursa zilizopo
- Katika Kanda zote mikutano hiyo ilihudhuriwa na wakulima, viongozi wa serikali, sekta binafsi, vyama vya wakulima, taasisi za fedha,washika wa maendeleo n.k

# Kanda za uzalishaji

- Kagera- Mkoa wa Kagera
- Kigoma- Mkoa wa Kigoma
- Mara- Mkoa wa Mara na Mwanza
- Arusha- Mkoa wa Arusha na Manyara
- Kilimanjaro- Mkoa wa Kilimanjaro na Tanga
- Ruvuma- Mkoa wa Ruvuma
- Iringa- Mkoa wa Iringa na Njombe
- Mbeya- Mkoa wa Mbeya na Katavi na Rukwa

# Taarifa ya Maazimio ya Kanda

- Kanda zilijadili na kuazimia maazimio mbalimbali,

Maazimio jumla yaliyopitishwa katika kanda zote ni;

I. H/Wilaya ziendee kutenga asilimia 20 ya mapato ya ushuru kwenye kahawa kwa ajili ya shunguli za kuendeleza zao
II. Serikali itekeleze ahadi ya kutoa ruzuku kwa wakulima wa kahawa

# Taarifa ya kanda ya Mbeya

Pamoja na mazimio mengine waliazimia yafuatayo;

- Bodi iendele na zoezi la kupata mchanganuo wa gharama za kuanzisha mnada wa kahawa Mbeya na kuziwasilisha kwa wadau.
- Serikali isadie katika kupunguza kodi zinazotozwa katika zao la kahawa
- Serikali ilete mrejesho kuhusu suala la kuanzishwa kwa mfuko wa kinga ya bei katika zao la kahawa
- Zoezi la upimaji wa afya ua udongo liendee na taarifa iwasishwe kwenye sekretariet ya Mkoa.

# Taarifa ya kanda ya Ruvuma

- Pamoja na mazimio mengine waliazimia yafuatayo;
- H/Wilaya na wadau wengine wachangie katika ununuziwa CPU na kukarabati zile zisizofanya kazi
- H/Wilaya zichukue hatua ya kukomesha biashara ya magoma/kuuza kahawa zikiwa shambani
- Wadau walikubaliana kuongeza kasi ya ujenzi wa maghala ya kuhifadhi kahawa
- H/Wilaya zinatakiwa kuharakisha utaratibu wa kutoa hati miliki kwa mashamba ya kahawa

# Taarifa ya kanda ya Kagera

- Kanuni za kahawa zirekebishwe ili madaraja yote ya kahawa ya Robusta yaruhusiwe kuuzwa kwa *Direct export*
- Halmashauri za wilaya zisimamie sheria za udhibiti wa ubora wa kahawa kuanzia uzalishaji mpaka masoko
- Wadau wote wanaochangia katika kuendeleza zao la kahawa na kudhibiti magendo watambuliwe na michango yao itolewe ufafanuzi wa matumizi

# Taarifa ya kanda ya Kigoma

- Kutokana na kuwepo kwa mvutano kati ya H/wilaya na vyama vya ushirika juu ya ulipaji wa ushuru wa zao la kahawa , Pande hizo zikutane na kukubalina juu ya kiwango cha ushuru kwa maslahi ya wote.
- Bodi ya kahawa ifungue tena ofisi ya Kigoma ili kusogeza huduma za bodi kwa wadau.
- H/wilaya ziendee kusimamia azimo la mkoa la kila kaya kupanda miti kahawa isiopungua 300 .
- Bodi ya kahawa itoe mafunzo kwa wakaguzi wa kahawa ili waweze kufanya kwa ufanisi kazi ya usimamizi wa sheria ya kahawa.

# Taarifa ya kanda ya Kiliamanjaro

- H/wilaya zitunge sheria ndogondogo za kuhakikisha wawekezaji waliowekeza kwenye mashamba ya makubwa ya kahawa hawabadilishi matumizi ya mashamba yao
- Wakaangaji na wadau wengine wa kahawa waendelee na uhamasishaji wa unywaji wa kahawa kwa njia mbalimbali ili kuwafikia wanywaji kahawa vijijini
- H/wilaya zianzishe kampeni na vilabu vya kahawa kwa vijana. Kila H/wilaya iwe na vilabu visivyopungua vitatu.

# Taarifa ya kanda ya Arusha/ Manyara

- Taarifa ya mapato na Matumizi ya Mfuko wa maendeleo ya zao iwasilishwe kwenye mikutano ya Kanda
- Wataalam kutoka TPRI waalikwe kwenye mikutano ya wadau ili watoe elimu kuhusu matumizi bora ya viuatilifu
- Juhudi zaidi zifanyike kuwahamasisha vijana kushiriki kwenye fursa za kibiashara zilizopo kwenye kahawa Mf. Kukaanga na kuuza kahawa ili kukuza soko la ndani

# Taarifa ya kanda ya Iringa/Njombe

Pamoja na mazimio mengine waliazimia yafuatayo;

- H/Wilaya zitoe taarifa na takwimu zinazoonyesha hali ya utekelezaji wa malengo yaliyowekwa
- Bodi ya kahawa na H/wilaya ziweke mkakati wa kupata vyanzo vingine vya fedha kwa ajili ya maendeleo ya zao
- Taarifa ya utekelezaji wa mkakati wa maendeleo ya kahawa itolewe katika vikao vinavyokuja

# Asante
# kwa nisikiliza